AJALI

# Ajali za barabarani bado janga kwa taifa

Na Sagini Hamis

SABABU za kibinadamu zimetajwa kuwa chanzo kikubwa cha ajali za barabarani nchini, zikichangia asilimia 97.1 ya ajali zote kwa mwaka 2024 zikihusisha mwendokasi, uzembe wa madereva na uendeshaji hatarishi wa waendesha pikipiki.

Sababu zingine zimetajwa kuwa ni ubovu wa magari, uliosababisha asilimia 2.2 ya matukio na sababu za kimazingira kama vile miundombinu mibovu ya barabara na moto zilizochangia asilimia 0.7 ya ajali zote.

Hayo yamebainishwa katika Ripoti Rasmi ya Uhalifu na Matukio ya Barabarani kuanzia Januari hadi Desemba, 2024 iliyotolewa na Jeshi la Polisi na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) iliyotolewa Aprili, 2025.

Katika ripoti hiyo, ajali za barabarani 1,520 ziliripotiwa Tanzania Bara kwa kipindi hicho huku idadi hiyo zilitofautiana na matukio 21 kulinganisha na ajali 1,541 zilizotokea katika muda kama huo mwaka 2023 na kuonyesha kupungua matukio ya ajali kwa asilimia 1.4.



Lori la mizigo likiwa limeteketea kwa moto, baada ya kuacha njia na kugonga nyumba katika eneo la Wazo, Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: JOHN BADI**

Pia takwimu hizo zinaonesha ajali 1,005 zilikuwa mbaya zaidi na zilisababisha vifo 1,521 mwaka 2024, ikiwa ni ongezeko la vifo 34 kulinganisha na ajali 987 zilizosababisha watu 1,487 kupoteza maisha mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 2.3.

Aidha, ripoti hiyo inabainisha kwamba ajali za pikipiki bado pasua kichwa kwa Tanzania. Katika mwaka 2024, kulikuwa na ajali za pikipiki 383 sawa na ongezeko la asilimia 2.4 kulinganisha na ajali 374 mwaka 2023. Ajali hizo zilisababisha vifo vya watu 341 na wengine 352 kujeruhiwa.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, mikoa iliyoathirika zaidi kwa ajali za pikipiki mwaka 2024 katika mikoa maalum ya kipolisi na idadi ya ajali kwenye mabano ni Temeke (35), Kinondoni (31), Dodoma (27), Lindi (26) na Mwanza 23.

Pia ripoti hiyo imetaja makosa mbalimbali ya usalama barabarani ambapo katika kipindi cha miezi 12 ya mwaka 2024, makosa 3,055,560 yalirekodiwa na kuonesha punguzo la asilimia 2.4 kutoka makosa 3,130,731 mwaka 2023.

Katika takwimu za makosa hayo mkoa wa kipolisi Ilala umeongoza kwa kuwa na makosa 382,613 ikifuatiwa na Kinondoni (329,951), Temeke (209,755), Morogoro (174,895) na Pwani (163,752).

Mikoa iliyoripotiwa kuwa na makosa machache ni mikoa mingine yenye makosa machache ni Rufiji (32,059) na Mara (37,970), Katavi (26,115), Tarime/Rorya (29,497) na Simiyu (30,848).

Kuhusu utekelezaji wa sheria, ripoti inaonesha kwa wastani kila askari wa usalama barabarani alisimamia makosa 810 mwaka 2024 huku Dar es Salaam ikiwa na mzigo mkubwa zaidi wa kazi kwa uwiano wa askari mmoja kwa kusimamia makosa 1,561.

Mikoa mingine yenye uwiano mkubwa wa makosa kwa askari mmoja ni Shinyanga (1:1,218) na Mbeya (1:1,204) huku ikionesha mahitaji makubwa ya rasilimali watu katika maeneo hayo.

Vilevile, ripoti hiyo imesema, mikoa yenye mzigo mdogo kwa askari ni Katavi (1:534), Kigoma (1:446) na Simiyu (1:454), na kuonesha uwezo tofauti wa utendaji wa askari katika maeneo mbalimbali nchini.

Kadhalika kupitia ripoti hiyo, Jeshi la Polisi Tanzania linaendelea na operesheni mbalimbali za usalama barabarani kupambana na makosa na kuongeza usalama kwa kuimarisha doria na utekelezaji wa sheria ili kupunguza ajali.

Pia imetaja mikakati maalum inayohusisha ukaguzi mkali wa basi za abiria na magari vituoni kabla ya safari pamoja na udhibiti wa mwendokasi kwa kutumia mfumo wa Vehicle Tracking System (VTS).

Aidha, jeshi hilo limesema litaendelea kuipa kipaumbele "Elimu Endelevu ya Usalama Barabarani" kwa watumiaji wote wa barabara ikihusisha madereva, waendesha pikipiki, watembea kwa miguu na waendesha baiskeli, ili kujenga uelewa na utiifu wa sheria.

Vilevile, ripoti hiyo imependekeza kuwa ili kupunguza ajali, kunahitaji mikakati thabiti, ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo mafupi kwa waendesha pikipiki na kuwahamasisha kujisajili katika Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Ardhini (LATRA).

Mambo mengine yanayopendekezwa ni kuhamasisha matumizi ya kofia ngumu, leseni halali, kukata bima na kutobeba abiria zaidi ya mmoja kwenye pikipiki.

CS CamScanner

Nipashe Ijumaa 18 July 2025 PG 18 (6)

# Madereva waagizwa kuzingatia sheria barabarani

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MADEREVA wa mabasi ya abiria kati ya Jiji la Mbeya na mikoa mingine, wameagizwa kuzingatia sheria za usalama barabarani ili kuepuka ajali, vifo vya watu, majeruhi na uharibifu wa mali.

Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Mbeya, Notker Kilewa alitoa agizo hilo jana wakati akifanya ukaguzi wa mabasi katika Kituo Kikuu cha Mabasi Mkoa wa Mbeya.

Kilewa alisema kuwa Jeshi la Polisi linaendelea na oparesheni za kukamata nagari kwa makosa ya usalama barabarani ikiwemo mwendokasi na kulazimisha kuyapita magari mengine kwenye maeneo ambayo hairuhusiwi.

"Leo tupo hapa kwa lengo la kutoa elimu na kuwakumbusha madereva kutii sheria za usalama barabarani bila shuruti, kuepuka kufanya makosa hatarishi na kuzidisha abiria," alisema.

Kilewa, alisema ajali nyingi chanzo ni uzembe wa madereva na kuwataka kuepuka vitendo hatarishi kwa kuwa vinagharimu maisha ya watu baada ya ajali kutokea.

Alisisitiza kuwa madereva watakaokamatwa kwa makosa ya usalama barabarani, wataendelea kuchukuliwa hatua kwa kupelekwa mahakamani na kufungiwa leseni zao.

Hata hivyo, Kilewa, aliwataka wamiliki kuhakikisha wanayafanyia matengenezo ya mara kwa mara ya mabasi yao ili kuepuka kuwa chanzo cha ajali.

Mwenyekiti wa Kamati ya Usalama Barabarani Mkoa wa Mbeya, Rajabu Ghuliku, aliwataka madereva na makondakta kuheshimu haki za abiria kwa kutimiza wajibu wao wa kutoa huduma bora ya usafirishaji.

Ghuliki, alisema madereva wanatakiwa kuhakikisha wanawafikisha abiria kwenye maeneo yao wakiwa salama na ubora wa huduma wanazotoa.

Alisema Mkoa wa Mbeya bila ajali inawezekana endapo wadau wote wa usafirishaji wataungana kukemea ukiukwaji wa sheria na taratibu.

"Sisi tuwaombe abiria wawe wepesi wa kutoa taarifa pale wanapobaini kuwa dereva ama kondakta anafanya vitendo ambavyo vinakiuka haki zao," alisema Ghuliku.

Akizungumza kwa niaba ya wenzake mmoja wa madereva wa mabasi hayo, Prosper Kilongo, alisema tatizo la mwendokasi kwa sasa limepungua kutokana na mabasi kufungwa vidhibiti mwendo (VTS) kutoa taarifa endapo mwendo umezidi.

Jeshi la Polisi Mkoa wa Mbeya linaendelea na utaratibu wa kufanya ukaguzi wa magari kabla ya kuanza safari na kutoa elimu ya usalama barabarani kwa madereva na abiria ili kuwajengea uelewa.

# Madereva wanaotumia vilevi hawana nafasi ya kuingia barabarani – DCP Kashai

NA ISSA MWADANGALA

**KATIKA jitihada za kuimarisha usalama wa barabarani, Mkuu wa Usalama Barabarani Nchini, Naibu Kamishna (DCP), Frasser Kashai, ametoa onyo kwa madereva wanaoendesha magari kutoka Dar es Salaam kuelekea nchi za kusini mwa Afrika wanaOtumia vilevi hawatokuwa na nafasi ya kuendesha vyombo vya moto kwani wanaweza kuleta madhara kwa watumiaji wengine wa barabara.**

Akizungumza katika kituo cha ukaguzi wa magari kilichopo eneo la Chimbuya, wilaya ya Mbozi mkoani Songwe, DCP Kashai aliwakumbusha madereva umuhimu wa kuendesha kwa uangalifu na kwa kuzingatia sheria za usalama barabarani ili kuepuka ajali zinazoweza kuzuilika.

"Madereva wanaotumia vilevi hawana nafasi ya kuendesha vyombo vya moto na kuingia navyo barabarani kwani wanaweka maisha yao na ya watumiaji wengine wa barabara katika hatari kubwa, jambo hilo hatutalivumilia wala kulifumbia macho na tutachukua hatua kwa wale wote wanaotenda kosa hilo ikiwa ni pamoja na kuwafungia leseni zao," alisema DCP Kashai kwa msisitizo.

Naye Afisa Mnadhimu wa Polisi kutoka Kamisheni ya Operesheni na Mafunzo, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP), Abdi Isango, alieleza kuwa Jeshi la Polisi linaendelea na msako mkali dhidi ya madereva wazembe, na alisisitiza kuwa ukaguzi unaofanyika katika vituo mbali mbali unalenga kuwatambua na kuwazuia wanaokiuka taratibu na sheria za usalama barabarani.

SACP Isango aliwahimiza madereva hao kushirikiana na Jeshi la Polisi kutekeleza majukumu yao kwa kufuata michoro, alama na sheria za usalama barabarani ikiwa ni pamoja na kuzingatia udereva wa kujihami na kuwa mabalozi wa usalama barabarani.

Jeshi la Polisi linaendelea kutoa elimu ya masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na umuhimu wa kufuata sheria za usalama barabarani ili kuhakikisha barabara za Tanzania zinakuwa salama kwa kila mtumiaji.

CamScanner